N11/2/ABSWA/HP1/SWA/TZ0/XX/T

88112388

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Friday 11 November 2011 (afternoon)
Vendredi 11 novembre 2011 (après-midi)
Viernes 11 de noviembre de 2011 (tarde)

1 h 30 m

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.



© International Baccalaureate Organization 2011

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# CHUKUA TENDA!
# TUNATAFUTA MASHIRIKA YANAYOWEZA KUPATA NA KUWASILISHA MADINI KWA BEI BORA

Baraza la Jiji la Nairobi linayaalika mashirika yanayoweza kupata na kuwasilisha madini yafuatayo:

- **i. WSD/1/2010- Madini ya Chumvi**
- **ii. WSD/2/2010- Magadi Soda**
- **iii. WSD/3/2010- Unga wa Klorini**
- **iv. WSD/4/2010- Maji ya Klorini**

Wanaokusudia kuwasililisha madini wanaombwa wapokee maelezo husika kutoka kwa afisi ya Meneja Msimamizi, Idara ya Mifereji na Maji, City Hall Annexe, orofa ya kwanza mlango nambari 115 na walipe shilingi 5000 pesa ambazo hazitarudishwa. Maombi yawekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri huku ikiwa na jina la ombi la madini na la mkataba na kutumbukizwa katika sanduku la maombi, Afisi ya Karani, City Hall, Mlango nambari 105, na iwapo barua hiyo itatumwa kupitia kwa njia ya Posta iandikwe kwa:

**Karani wa Baraza la Jiji,**
**Jiji la Nairobi,**
**S.L.P 30075,**
**NAIROBI.**

Ili kumfikia kabla ya **saa sita mchana** mnamo Novemba 11, 2011. Maombi yote yatafunguliwa muda mfupi baadaye katika Chumba cha Mikutano cha Baraza hilo kilichoko ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Nairobi, Orofa ya kwanza mbele ya wanakamati wanaohusika na maombi watakaohudhuria. Maombi yote lazima yaandamane na dhamana zilizoelezwa katika tangazo. Baraza la Jiji halina jukumu la kupokea na kutazama ombi kwa orodha maalum.

JOHN MALIMOTO

KARANI WA BARAZA LA JIJI LA NAIROBI


*Taifa Leo* (2010)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

# WANYAMA KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI



Watu wengi kutoka Afrika ya Mashariki wanapenda kufuga wanyama. Miongoni mwa wanyama hao ni mbwa, paka, punda, farasi, ng'ombe, mbuzi na kondoo. Mbwa aghalabu hufugwa ili wakati wa usiku walinde nyumba za mabwana wao. Paka hufugwa kwa ajili ya kushika panya kwa kuwapaka ni adui mkubwa wa panya. Baadhi ya watu hufuga paka kwa sababu ni mnyama mzuri mwenye manyoya mororo na hupendeza akiwamo nyumbani. Punda hufugwa kwa ajili ya kubebeshwa mizigo. Farasi hupandwa au hufanyishwa kazi mashambani. Ng'ombe na mbuzi hufugwa na jamii nyingi ulimwenguni. Katika Afrika ya Mashariki makabila mengi hufuga ng'ombe na mbuzi kwa maana wanyama hawa ni mali. Utajiri wa mtu hupimwa kwa kadiri ya idadi ya mifugo yake. Kati ya makabila yaliyoko Afrika Mashariki yanayofuga ng'ombe na mbuzi ni Wamasai, Wasomali, Waturkana, Wakamba na Wagogo. Kwenye sehemu za baridi kondoo hufugwa kwa wingi kwa ajili ya manyoya yao. Manyoya hayo yakikatwa huitwa sufu ambayo hutumiwa kutengenezea nguo za joto.

Ingawa wanyama ni wenye manufaa na msaada kwa wanadamu, lakini inasikitisha kuona mara kwa mara wakitendewa mabaya. Punda hubebeshwa mizigo mizito mno na kuendeshwa mwendo mrefu huku akipigwa kwa fimbo vikali ili aende mbio. Watoto watundu huwatupia mawe mbwa na paka kama mchezo tu. Hawafahamu kuwa mchezo wao unawaletea wanyama hawa mateso na maumivu. Kuwatesa wanyama hivi si haki kabisa. Wanyama ni mabubu, hawawezi kusema ili wajitetee. Hawawezi kusema wanaumia wanapobebeshwa mizigo mizito migongoni mwao. Wakiwa na njaa au kiu hawana uwezo wa kuomba chakula. Wanapoumizwa au kuvunjwa viungo na watoto watundu hawawezi kulalamika wala kuomba watibiwe.

Basi ni wajibu wetu tunapowaona watu wakifanyia wanyama vitendo vya ukatili kuwakataza, kwani wanyama hawa ni wapole na watii na wamethibitisha urafiki wao kwetu. Tusisahau kuwa wao ni kama sisi wanadamu. Wao na sisi ni viumbe wa Mungu.

Saidi *et al.*, *Kusoma na Kufahamu Kiswahili* (1998)



https://xtremepape.rs/


**KIFUNGU C**

# KAMPENI ZA BUNGE

Mulei aliongea huku akiinama chini kwenye chombo cha kuzungumzia. "Wananchi wenzangu, mgeni mashuhuri, mabibi na mabwana! Leo hii, mimi nimefika ili kuingiza mashilingi mifukoni mwenu. Mali sasa! Huu ndio utakaokuwa msemo wetu tangu leo. Si baada ya miaka kumi, wala sio ahadi tupu zisizo na msingi, bali ni hivi leo. Mali sasa!"

Kisha, yeye pamoja na umati, "Mali sasa! Mali sasa!" Naye Mulei akaendelea kusema, "mwaka ujao, tutahitaji kupewa sehemu fulani ya fedha kutoka kwa kodi tunayotoa. Ikiwa si hivyo, hatutatoa kodi yoyote." Umati ulimshangilia kwa nguvu alipomaliza kutamka maneno haya. "Wakati nitakapofika katika Baraza la kutunga sheria, yaani Bunge, sharti niwaonyeshe kwa vitendo wala sio maneno matupu peke yake. Ni lazima tuwe na skuli yetu ya sekondari. Serikali kuu ni lazima kutoa pesa na kuiendesha skuli yenyewe." Halafu Mulei alivua koti, akafungua shati na tai, kisha akatupa mikono juu. "Sisi tunahitaji hospitali mpya. Tunahitaji kitendo halisi. Tunapenda jambo fulani lifanywe sasa! Siyo ahadi tupu tunazopewa kila siku. Tunahitaji mshahara maradufu na unaofaa. Twapenda kupewa mshahara mara mbili kuliko tunavyopewa sasa."

"Toboa! Toboa!" Umati ukasema na kushangilia kwa furaha.



"Dhahabu mfukoni mwa kila mtu! Na kwa nini isiwe hivyo!"

Wakati wote huo halaiki ilizidi kushangilia kwa nyimbo, pamoja na msemo wao, "Mali sasa! Mali sasa!"

Baadhi ya wananchi walisimama wima na kusema, "Yafaa tumtume shujaa Mulei katika Bunge sasa. Ndiye pekee anayeweza kuharakisha mambo na kuyatimiza matakwa yetu."

Mulei alikuwa amekwisha kuwapanga watu foleni kwa uangalifu, huku na huko, hasa barobaro waliomwunga mkono, kusudi wapate kuufanya umati wote kushangilia. Hakulisahau neno lolote kati ya yote aliyotaraji kuyasema wakati huo.

J S Ndeti, *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani* (1983)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# ATHARI ZA ULEVI

Kuna majadiliano makali yanayoendelea kuhusu faida za ulevi au madhara yanayofungamana na tabia hii, hasa ikiwa umepindukia kiasi. Baadhi ya watu hudai kuwa tembo kidogo ni nzuri kwa afya na humletea mtu uchangamfu. Kwa mfano, mtu huonekana ni mwenye furaha na kupenda kuzungumza baada ya kunywa pombe kidogo. Pia ni njia rahisi ya kukutana na marafiki hasa kwenye vilabu vya pombe.

Kuna mawazo mengine kuwa manufaa yanayopatikana katika kunywa pombe ni machache ilhali madhara yanayopatikana ni makubwa. Marubani kwa mfano hawana ruhusa kugusa pombe saa nane kabla ya kuendesha ndege au wakati wowote wanapoendesha. Hili ni thibitisho kuwa tembo, hata kiasi kidogo, huathiri mizani ya binadamu. Na orodha ya madhara ya tembo, hasa kwa wale wanaopitisha kiasi, hayana hesabu. Afya ya mwenye kutumia huharibika.

Jamii nyingi huachwa katika hali ya mateso na watoto mara nyingi huharibiwa maisha yao na wazazi wanaodumu katika ulevi. Saa nyingi katika kazi huweza kupotea kwa sababu ya ulevi na maendeleo ya nchi kwa jumla kurudi nyuma.

Je, kuna haja ya kuwawacha watu mpaka wakafika kiwango hiki katika ulevi? Lakini si watu wote watumiao pombe wanaofika daraja hili tulilolieleza. Watu ni tofauti. Wengine huweza kujizuia nafsi zao na kunywa pombe kiasi kidogo tu. Lakini tukidadisi, tutagundua kuwa pombe ina mazoea ambayo si rahisi kuwachika. Mazoea haya ni sawa na mazoea ya ulevi mwingine kama vile mihadarati, bangi na sigara. Mbali na mazoea ya ulevi, kuna mazoea ya watu ambao baada ya alasiri hukutana kila siku katika vilabu vya pombe. Hapa huwa pana mazungumzo “matamu” na kwa sababu kila mmoja ana chupa yake ni vigumu kuweka kikomo cha unywaji wakati ambapo mazungumzo ya kufurahisha yanaendelea. Wake na watoto wao huwa wamesahauliwa majumbani.

S Mirza *et al*., *Kiswahili: Msingi wa Kusema, Kusoma na Kuandika* (2010)



https://xtremepape.rs/